LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

# UFIKIWAJI NA UPATIKANAJI WA HAKI KWA WATU WENYE ULEMAVU

Kwa Jamii Yenye Haki na Usawa

## Utangulizi

Sheria ya watu wenye ulemavu namba 10 ya mwaka 2009 inatoa haki ya watu wenye ulemavu kufikia na kupata huduma zote za jamii na kupata msaada stahiki kama vile wasomaji, wakalimani, lugha za alama na wasindikizaji.

### 1. Ulemavu ni nini?

Ni hali inayotokana na dosari mwilini au/na akilini ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuyaweza na hivyo kumletea mtu huyo kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii.

### 2. Mtu mwenye ulemavu ni nani?

Ni mtu ambaye mategemeo yake ya kupata, kumudu na kujiendeleza katika kazi yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ulemavu unaotambulika mwilini, akilini na/au mfumo wa mitazamo wa jamii dhidi ya mtu huyo.

Sheria inaondoa vizuizi vinavyowapata watu wenye ulemavu katika hali ya kuishi na kujitegemea kama wanavyotaka. Vizuizi vinakatazwa;

- Kwenye miundombinu hususani majengo ili kuwezesha ufikikaji kirahisi kwa watu wenye ulemavu;
- Kwenye huduma zote na maeneo ya umma na kwamba zitaweka viwango vya ufikikaji kwa watu wenye ulemavu;
- Kwenye upatikanaji habari na mawasiliano pia katika huduma za kielektroni.

### 3. Ufikiaji ni nini?

Ni ruhusa, njia au uwezo wa kupatikana. Katika maana pana, ufikiaji pia hujumuisha uwezo wa watu wenye ulemavu kupata mazingira, mifumo ya usafiri, habari na mawasiliano, teknolojia ya habari, vifaa na huduma nyinginezo za umma bila vikwazo.

### 4. Je kuna umuhimu gani wa kuondoa vizuizi kwa watu wenye ulemavu?

- Kuleta usawa katika upatikanaji na utumiaji wa miundombinu na huduma mbalimbali
- Kuwawezesha kujitegemea na kumudu kutembea wanavyotaka
- Kutunza afya na usalama wa watu wenye ulemavu
- Kutengeneza na kuendeleza faraja kwa watu wenye ulemavu

### 5. Ni mifano gani ya kuzingatia ili kuwezesha ufikiwaji au upatikanaji wa miundombinu na huduma kwa watu wenye ulemavu?

- Maegesho ya magari yaliyokaribu na milango ya kuuingilia
- Kuondoa vikwazo katika njia za kupita (mashimo, mawe, majani)
- Kusogeza huduma za jamii karibu na maeneo wanayoishi watu wenye ulwmavu
- Kuweka alama za watu wenye ulemavu barabani
- Kutengeneza miteremko hususan kwa ajili ya viti vya magurudumu
- Kuruhusu mwanga wa kutosha katika maeneo yote (mwanga wa jua na taa)
- Taarifa za dharura kutolewa katika

lugha inayoeleweka kwa makundi yote yenye ulemavu

- Vitendea kazi viwe kwenye urefu unaofikika
- madawati ya taarifa yanayofikika kirahisi
- ngazi ambazo ni salama na rahisi kutumia kibinafsi
- kupunguza umbali wa usafiri/ kutembea ili vitengo mbalimbali katika jengo moja
- nafasi za kutosha katika majengo kuwezesha mizunguko ya watu wenye ulemavu na vifaa au wasaidizi wao (binadamu/wanyama)
- nafasi maalum zitengengwe kwa ajili ya kukaa au kupumzikia watu wenye ulemavu

### 6. Ni nini changamoto ya utekelezaji wa sheria na sera kuhusu ufikiwaji na upatikanaji wa miundombinu na huduma za jamii kwa watu wenye ulemavu?

- Ukosefu wa mafunzo kwa watu wenye ulemavu juu ya mazingira wezeshi, vifaa vya usaidizi, mifumo ya usafiri, habari na mawasiliano
- Ufatiliaji dhaifu wa utekelezaji wa miongozi inayohusu upatikanaji wa huduma na ufikiwaji wa miundombinu
- Ukosefu wa wataalamu wa kutosha wenye uzoefu na sifa za kiufundi kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu
- Elimu duni ndani ya jamii inayoletwa na mitazamo tofauti juu ya watu wenye ulemavu
- Ukosefu wa tafiti zinazojitosheleza kwa ajili ya kupanga mikakati juu ya masuala ya watu wenye ulemavu
- Ukosefu wa sera na mikakati jumuishi
- Utekelezaji kuonekana kama ghali hususan katika taasisi binafsi
- Ukosefu wa mafunzo ya kutosha kwa wafanyakazi katika taasisi za umma na wale wanaotoa huduma kwa jamii

### 7. Je ni nini wajibu wa nchi katika kuhakikisha kwamba vizuizi hivyo vinaondolewa?

- Kuendeleza, kueneza na kufuatilia utekelezaji wa viwango na miongozo kuhusu upatikanaji wa huduma kwa ajili umma;
- Kuhakikisha kuwa huduma za taasisi zote binafsi zinawafikia watu wenye ulemavu;
- Kutoa mafunzo kwa wadau juu ya matatizo ya watu wenye ulemavu katika upatikanaji wa huduma
- Kuweka sehemu zinazohudumia umma alama kwa maandishi ya Nukta Nundu na kwa njia nyingine zinazosomeka na kueleweka kirahisi;
- Kutoa visaidizi halisi na wasaidizi (waongozaji, wasomaji na wakalimani) ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kuyafikia na kuyatumia majengo na huduma nyingine za umma;
- Kutoa aina nyingine za usaidizi ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata habari/taarifa;
- Kuhamasisha upatikanaji wa aina mpya za teknolojia na mifumo ya habari na mawasiliano kwa watu wenye ulemavu
- Kuendeleza, kuzalishaji na kusambaza teknolojia na mifumo ya habari na mawasiliano ili zipatikane kwa gharama nafuu.

### 8. Je ni nini wajibu wa jamii katika kuhakikisha kwamba vizuizi hivyo vinaondolewa?

- Kuwaheshimu watu wenye ulemavu kimaumbile na kiakili kama watu wengine;
- Kuwasaidia kushiriki na kujumuishwa katika shughuli mbalimbali kwenye jamii zao;
- Kutokuwabagua watu wenye ulemavu;
- Kupigana dhidi ya Imani potofu na chuki kuhusu watu wenye ulemavu;
- Kutoa uangalizi, kuwasaidia na kuwatunza watu wenye ulemavu;

### 9. Ni nini LHRC inafanya?

- Kutoa elimu na mafunzo kwa jamii ili waweze kutambua na kutetea haki za watu wenye ulemavu
- Kutoa msaada wa kisheria katika masuala yanayohusu uvunjifu wa haki za watu wenye ulemavu
- Kushawishi serikali kutunga na kurekebisha sheria zinazohatarisha haki za watu wenye ulemavu

### 10. Wito

- Mtu mwenye ulemavu ni sawa kama mtu mwingine yeyote na anastahili kufurahia haki zake katika usawa na ubora uleule kama mtu asiye na ulemavu.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
**(MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
**S. L. P.** 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz Tovuti: www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
**S. L. P.** 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva,
Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
**S. L. P.** 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D,
**S.L.P** 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**@humanrightstz**

**HakiTV**

**Kwa Jamii Yenye Haki na Usawa**